# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI NA SITA

**16 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA AROBAINI NA SITA - TAREHE 16 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**585 MHESHIMIWA DANIEL TLEMAI AWACK (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Wodi ya Wazazi na Jengo la Maabara Kituo cha Afya Oldeani Karatu.

**586 MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Zahanati za Buhulyu, Mogwa, Mwanzwilo na Gulyambi - Bukene zitaanza kutoa huduma.

**587 MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa kupandisha hadhi Vituo vya Afya na Zahanati zinazookoa maisha ya Wananchi nchini.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**588 MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Zimamoto katika Halmashauri ya Mji wa Bunda.

## WIZARA YA UJENZI:

## 589 MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itatangaza tenda ya ujenzi wa Km 20 kwa kiwango cha lami Barabara ya Kolandoto - Kishapu hadi Mwangongo.

## WIZARA YA FEDHA:

## 590 MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua masharti kandamizi kwa Wawekezaji wa ndani kama kukadiria na kulipa kodi kabla ya kuanza biashara.

## 591 MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, changamoto zipi zinazorotesha ukusanyaji wa mapato katika mfumo mpya wa kuchakata Kodi ya Forodha ambao ni "*single window*".

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**592 MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina Sera za kuwawezesha Wanawake Wajasiriamali kutumia Teknolojia ya Habari kuongeza ufanisi wa biashara zao.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**593 MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Geti la kuingilia Watalii Hifadhi ya Mto Ugala Wilaya ya Urambo litawekwa.

## WIZARA YA MAJI:

**594 MHESHIMIWA KATANI AHMAD KATANI (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itawalipa fedha Wakandarasi wa miradi ya maji kutokana na miradi mingi kutokamilika kwa kukosa malipo kwa wakati.

**595 MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wilaya ya Kakonko itakuwa na Wakala wa Mamlaka ya Maji Mjini katika Mji wa Kakonko.

**WIZARA YA KILIMO:**

**596 MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto zilizojitokeza wakati wa ununuzi wa mbegu za ruzuku kwa Wakulima nchini.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**597 MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itamuomba Mwekezaji wa Chai Rungwe kuachia ardhi ambayo haitumii kwa Wananchi.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2025 *(The Finance Bill, 2025).*

## V. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**16 JUNI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA